JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA UCHUKUZI

MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI

# TAARIFA KWA UMMA

## RUHUSA KWA MABASI YA DAR – LINDI – MTWARA KUPITA KWA DHARURA SONGEA – MAKAMBAKO – IRINGA

***Dar es Salaam, Tarehe 06 Aprili, 2025***

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini, inatoa taarifa kwa Umma kuwa, kufuatia mvua zinazoendelea kunyesha mikoa ya Kusini – Mashariki mwa Tanzania, kumetokea uharibifu wa barabara ya mchepuko iliyokuwa ikitumika kupisha ujenzi unaoendelea wa daraja eneo la Somanga - Mtama, Wilaya ya Kilwa, Mkoani Lindi ambapo barabara hiyo imefungwa kwa muda na Wakala wa Barabara Nchini (TANROADS) kuanzia jioni ya Jumapili, tarehe 6 Aprili, 2025.

Kutokana na changamoto hiyo**, Mamlaka inatoa ruhusa kwa wasafirishaji ambao ratiba zao zimeathirika na uharibifu huo, kutumia njia mbadala kwa dharura kati ya Dar es Salaam – Lindi – Mtwara – Masasi – Tunduru kupitia Songea, Makambako na Iringa. Dharura hii itamalizika baada ya barabara iliyofungwa kwa muda kuanza kutumika.**

Rai inatolewa kwa madereva watakaopita njia ambazo hawana uzoefu nazo, wachukue hadhari zaidi, hususan, wanapopita maeneo yenye miteremko au milima na wasipitishe mabasi katika barabara zilizojaa maji. Katika njia hizo mbadala, wasafirishaji wazingatie viwango vya nauli kulingana na umbali kama vinavyooneshwa katika majedwali ya nauli elekezi zilizotolewa na LATRA ambazo pia zinapatikana kwenye tovuti www.latra.go.tz au **LATRA App** kwa simu janja za Android.

Mamlaka inawakumbusha watoa huduma wote kuzingatia Sheria na Kanuni za huduma wanazotoa, ikiwemo kutumia mfumo wa tiketi za kielektroni. Abiria wanakumbushwa kutoa taarifa za changamoto za usafiri kwa kupiga simu bila malipo namba 0800110019/20 inayofanya kazi siku zote saa 24 au kupitia mfumo wa e-mrejesho.

Digitally Signed By Salum PAZZY
Sun Apr 06 13:36:42 EAT 2025

Salum PAZZY

**Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano**